# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI (TASAF III) KATIKA MKOA WA MWANZA

Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ni mojawapo ya mradi katika Programu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Awamu ya Tatu (TASAF III), ulizinduliwa Mkoani Mwanza Oktoba 2014 na utekelezaji wake ulianza Julai 2015. Lengo la Mpango ni kuziwezesha Kaya maskini kuongeza kipato, fursa na kuongeza ufanisi katika matumizi ya chakula, afya na elimu. Kimkoa Mpango huu unatekelezwa katika Wilaya 7 za Nyamagana, Ilemela, Magu, Kwimba, Misungwi, Sengerema na Ukerewe.

## HALI YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA TASAF AWAMU YA TATU

**S**hughuli zilizokwishatekelezwa na zinazoendelea kutekelezwa na Mpango huu ni pamoja na:-

(i) **Utambuzi na Uandikishaji wa Kaya Maskini**

Utambuzi na uandikishaji wa Kaya maskini ulihusisha jumla ya Mitaa 142 na vijiji 362 na kuacha Mitaa 205 na Vijiji 122 ambayo haijaanza kutekeleza Mpango huu. Jumla ya Kaya 75,142 zilitambuliwa na kupitishwa katika mfumo wa uhakiki wa Kompyuta kwa kutumia vigezo vya utambuzi vilivyowekwa hivyo, jumla ya Kaya 62,412 ziliandikishwa. Aidha, kutokana na zoezi la kufuta kaya zisizo na sifa lililofanyika mwezi Mei, 2016 na kuendelea, idadi ya Kaya imepungua na kubaki 55,829 kama inavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:-

**Jedwali Na 1: Idadi ya kaya zilizopo baada ya zoezi la uhakiki**

| Na. | Wilaya | Vijiji/ Mitaa iliyohusika | Idadi ya Kaya zilizotarajiwa kuandikishwa | Idadi ya Kaya zilizoandikishwa | Kaya zilizobaki baada zoezi la kufuta zisizo na sifa (Januari, 2018) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Kwimba | 86 | 10,299 | 10,019 | 9,179 |
| 2. | Magu | 54 | 6,133 | 5,940 | 5,588 |
| 3. | Misungwi | 60 | 12,680 | 9,395 | 8,641 |
| 4. | Ilemela | 69 | 11,613 | 4,807 | 3,912 |
| 5. | Nyamagana | 73 | 10,512 | 8,502 | 7,701 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 6. | Sengerema | 107 | 17,472 | 17,162 | 14,477 |
| 7. | Ukerewe | 55 | 6,703 | 6,587 | 6,331 |
| **Jumla** | | **504** | **75,412** | **62,412** | **55,829** |

*Chanzo: Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mkoa wa Mwanza 2018*

Hata hivyo, zoezi la kuondoa kaya zisizo na sifa ni endelevu.

(ii) **Uhawilishaji wa Fedha kwa Kaya Maskini**:

Shughuli ya uhawilishaji wa fedha kwa Kaya Maskini kwa mwaka wa fedha wa 2015/16, 2016/2017 na 2017/2018 katika kipindi cha Julai hadi Januari imefanyika kwa awamu kumi na sita ambapo Mkoa umepokea jumla ya shilingi **42,982,195,066.93** toka TASAF makao makuu kwa ajili ya kutoa ruzuku kwa walengwa pamoja na shughuli za usimamizi na ufuatiliaji katika ngazi ya Mkoa, Halmashauri, Mitaa/ Vijiji na Kata.

(iii) **Utekelezaji wa Miradi ya Kutoa Ajira za Muda kwa Walengwa**

Mpango huu unaziwezesha kaya maskini kujiongezea kipato kwa kutoa ajira za muda katika vipindi vya muwambo kwa mwaka, kaya zenye watu wenye uwezo wa kufanya kazi hupewa ajira na kufanya kazi katika miradi iliyoibuliwa na jamii. Katika miradi hii kiasi cha asilimia 75% ya fedha za utekelezaji hulipwa walengwa na asilimia 25% hutumika kulipa gharama za kuendeshea mradi.

Halmashauri ya wilaya ya Misungwi ni Halmashauri pekee katika Mkoa inayotekeleza miradi ya Utoaji Ajira za Muda. Jumla ya vijiji 51 vinatekeleza miradi ya utoaji ajira za muda. Kwa mwaka wa fedha 2016-2017 jumla ya miradi 58 imetekelezwa ambapo miradi hiyo imegawanyika katika makundi matatu ambayo ni miradi 28 ya miti , miradi 6 ya uchimbaji wa visima vifupi na miradi 17 ya uchimbaji na ukarabati wa marambo, jumla ya shilingi **854,647,930.68** zimelipwa kwenye kaya 7,035 ikiwa ni ujira wa kushiriki katika miradi hiyo. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 jumla ya miradi 79 imeibuliwa ambayo imegawanyika katika makundi matatu ambayo ni miradi ya 20 upandaji miti, miradi 27 ya ukamilishaji na uchimbaji wa malambo na miradi 32 ni ya uchimbaji wa visima vifupi vya maji. Jumla ya shilingi **30,616,700.00** zimetolewa kwa ajili ya uibuaji wa miradi na shilingi **26,240,500.00** zimetolewa kwa ajili ya mafunzo ya wasimamizi wa miradi, utekelezaji

unaendelea. Zifuatazo ni baadhi ya picha za utekelezaji wa miradi ya Ajira za Muda Wilayani Misungwi:



Ukarabati wa lambo Kijiji cha Kijima



Ujenzi wa lambo Kijiji cha Inonelwa



**Shamba la miti kijiji cha Magaka**

## MAFANIKIO YA TASAF AWAMU YA TATU

Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mpango huu tangu uanze kutekelezwa ni pamoja na:-

i) Kaya zilizotambuliwa na kuandikishwa kwa kuzingatia vigezo zinaendelea kupokea malipo ya ruzuku kila baada ya miezi miwili.

ii) Mpango umewezesha kuwepo kwa ongezeko la mahudhurio ya wanafunzi shuleni na watoto wenye umri wa kuhudhuria huduma za kliniki kwa kuzingatia ruzuku inayotolewa kwa kutimiza masharti ya kuhudhuria shule na kliniki.

iii) Walengwa wengi walioko katika Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini wameweza kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) na kulipa kiingilio cha Tsh. 10,000/- kutoka katika ruzuku zao ili wapate matibabu kwa mwaka mzima kama inavyoonyeshwa katika jedwali namba 2 hapa chini:-

**Jedwali Na.2: Kaya zilizojiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) hadi Mwezi Januari, 2018**

| Na. | Wilaya | Idadi ya Kaya maskini kufikia Disemba, 2017 | Idadi ya Kaya zilizojiunga na CHF | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kwimba | 9,179 | 7,559 | 82 |
| 2. | Misungwi | 8,641 | 6,375 | 73 |
| 3. | Nyamagana | 7,701 | 1,475 | 19 |
| 4. | Sengerema | 14,477 | 12,046 | 83 |
| 5. | Magu | 5,588 | 3,650 | 65 |
| 6. | Ukerewe | 6,331 | 5,656 | 89 |
| 7. | Ilemela | 3,912 | 0 | 0 |
| **Jumla** | | **55,829** | **36,761** | **65** |

*Chanzo: Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mkoa wa Mwanza 2018*

Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na TASAF zipo changamoto katika utekelezaji ambazo ni pamoja na:-

- Kuwepo kwa baadhi ya wananchi wenye sifa ya kuingizwa kwenye Mpango wa Kunusuru Kaya maskini, aidha uhitaji wa Vijiji/Mitaa iliyoachwa kuingizwa kwenye Mpango imekuwa ni tatizo pia
- Baadhi ya viongozi na watendaji kujaribu kufanya udanganyifu ili kujinufaisha au kuiba fedha za walengwa.

Hata hivyo hatua zimechukuliwa kutatua changamoto zilizojitokeza ikiwa ni pamoja na:-

- Kuendelea kufanya uhakiki wa taarifa za wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ili kupata taarifa sahihi za walengwa.
- Wale wote waliohusika kwa namna moja au nyingine kufanya udanganyifu wa fedha za walengwa wamechukuliwa hatua za kisheria kulingana na tuhuma kwa kila Wilaya.

- Mkoa umejipanga kuendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya kwa kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ili Mpango huu uweze kuleta matokeo chanya kwa walengwa kama ilivyokusudiwa. Zifuatazo ni picha mbalimbali zilizochukuliwa katika ufuatiliaji wa shughuli za TASAF



Timu ya ufuatiliaji ya Mkoa ikifanya mahojiano na Viongozi na walengwa kijiji cha Nyang'holongo Wilayani Misungwi



Mtaalam kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa akitoa ufafanuzi wa jambo kwa walengwa katika kijiji cha Shilanona Wilayani Kwimba.



Bw.Ladslaus Matata ni mnufaika (Juu ya mawe) akiwa na wataalam wa Sekretarieti ya Mkoa akionesha shughuli anayofanya baada ya kuwezeshwa na mradi wa TASAF Wilayani Ukerewe.



Kikao kazi kwa watendaji wa shughuli za TASAF cha Mkoa kilichofanyika Julai 1, katika Ukumbi wa Mkuu wa Mkoa. Kikao kilijumuisha Wakurugenzi, Maafisa Ufuatiliaji, Waratibu, Wahasibu na Timu ya Mkoa ya ufuatiliaji.



Wanafunzi wanaonufaika na Mpango ambao wanatimiza masharti ya Elimu Shule ya Msingi Nyamililo Wilayani Sengerema.



Watoto (miaka 0- 5) wanaonufaika na Mpango ambao wanatimiza masharti ya Afya wakipima uzito katika  Kituo cha Afya Sima Wilayani Sengerema.